

EFF'S SURVEILLANCE SELF-DEFENSE

# SIMU ZA RUNUNU: UPELELEZI KWENYE MAWASILIANO YA SIMU ZA RUNUNU

---

<https://ssd.eff.org/en/about-surveillance-self-defense>

**E** ELECTRONIC  
FRONTIER  
FOUNDATION **FF**



**LOCALIZATION LAB**

## Upelelezi kwenye Mawasiliano ya Simu za Rununu

Hapo awali, mitandao ya simu za rununu haikuundwa awali ili kutumia njia za kiufundi kulinda simu zinazopigwa na kupokelewa na wateja dhidi ya kusikilizwa. Hiyo ilimaanisha kwamba mtu yeyote aliye na aina sahihi ya kipokezi cha redio angeweza kusikiliza mawasiliano hayo ya simu.

Hali ni bora zaidi siku hizi kwa kuwa teknolojia za usimbaji fiche zimeongezwa kwenye viwango vya mawasiliano ya simu za rununu ili kujaribu kuzuia usikilizaji. Lakini nyingi za teknolojia hizi zimeundwa vibaya (wakati mwingine kwa makusudi, kwa sababu ya shinikizo la serikali kutotumia usimbaji fiche wenye nguvu). Zimesambazwa kwa njia isiyokuwa na usawa, kwa hivyo zinaweza kupatikana kwa mtoa huduma mmoja lakini si mwingine au katika nchi moja lakini si nyingine na wakati mwingine zimetokeleza isivyofaa. Kwa mfano, katika baadhi ya nchi watoa huduma hawawashi usimbaji fiche hata kidogo au wanatumia viwango vya kiufundi vilivyopitwa na wakati. Hii inamaanisha kuwa mara nyingi bado inawezekana kwa mtu aliye na aina sahihi ya kipokezi cha redio kudukua mawasiliano ya simu na ujumbe wa maandishi unaposambazwa hewani.

Mbinu salama zaidi ni kudhania kuwa mawasiliano ya simu ya kawaida na jumbe fupi za maandishi SMS hazijalindwa dhidi ya kusikilizwa au kurekodiwa. Ingawa maelezo ya kiufundi yanatofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka mahali pamoja hadi kwingine na mfumo mmoja hadi mfumo mwingine, ulinzi wa kiufundi mara nyingi ni dhaifu na unaweza kuepokwa katika hali nyingi.

Angalia [Mawasiliano na Wengine](#) ili ujifunze jinsi ya kutuma ujumbe mfupi na kuzungumza kwa usalama zaidi.

Hali inaweza kuwa tofauti unapotumia programu za mawasiliano salama kuwasiliana (iwe kwa sauti au maandishi), kwa sababu programu hizi zinaweza kutumia usimbaji fiche ili kulinda mawasiliano yako. Usimbaji fiche huu unaweza kuwa na nguvu zaidi na unaweza kutoa ulinzi wa maana zaidi. Kiwango cha ulinzi unaopata kutokana na kutumia programu salama za mawasiliano kuwasiliana kinategemea sana na programu unazotumia na jinsi zinavyofanya kazi. Swali moja muhimu ni iwapo programu ya mawasiliano hutumia usimbaji

fiche kutoka mwanzo hadi mwisho ili kulinda mawasiliano yako na kama kuna njia yoyote kwa mtengenezaji wa programu kutendua au kukwepa usimbaji huo.



## Maelezo zaidi

- [Kwanini Data za Jumla ni Muhimu](#)